



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

UNESCO, Umoja wa Ulaya na Washirika wa Taifa wa Urithi wa Mradi wa Uhifadhi na Uendelezaji wa Hifadhi za Urithi Tanzania wazindua Studio za Mwalimu Nyerere - Kumbukumbu ya Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika katika Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC)

UNESCO kwa kushirikiana na Wadau na Washirika wa Mradi wa Umoja wa Ulaya (EU); kwa ufadhili wa Mradi wa Uhifadhi na Uendelezaji wa Hifadhi za Urithi Tanzania, hususani Hifadhi ya Urithi wa Kiafrika, kwa pamoja watazindua Studio za Mwalimu Nyerere – zijulikanazo kama Kumbukumbu ya Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika. Uzinduzi huu utafanyika mnamo Ijumaa tarehe 27 Julai 2018 katika jengo la Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), lililopo Barabara ya Pugu jijini Dar es Salaam.

Ukarabati wa kituo hicho ulifanywa na UNESCO kupitia mradi wake unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya nchini wenye lengo la kuhakikisha ulinzi, uhifadhi na uhuishaji wa kumbukumbu za urithi za Tanzania pamoja na uhifadhi wa kumbukumbu za harakati za Ukombozi wa Afrika. Mradi huu unalenga kuhakikisha uendelevu wa utunzaji wa kumbukumbu za sauti na machapisho ya urithi kwa kuongeza uwajibikaji, upatikanaji na kukuza uratibu wa kusimamia urithi huu muhimu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Studio hii ni tunu muhimu ya urithi na eneo la kihistoria ambalo lilitumiwa sana katika zama za Ukombozi kama kituo cha utangazaji kikiwa na huduma za mifumo ya nje iliyowekwa mahususi kwa Harakati za Ukombozi wa Kusini mwa Africa. TBC (iliyojulikana kama Radio Tanzania) ilirusha hewani vipindi na kuajili waandishi wa habari kutoka karibu maeneo yote yaliyokuwa na harakati za ukombozi. Ukarabati huu ulifadhiliwa na UNESCO huku urejeshwaji wa kumbukumbu ukifadhiliwa na Umoja wa Ulaya, ambapo unawezesha vifaa hivyo kutumika kama sehemu ya Maktaba ya kudumu ya kuwasilisha/kuonyesha kumbukumbu za historia ya Ukombozi kupitia makumbusho ya redio na kuwezesha umma kujipatia nyaraka za Urithi. Kwa sasa, eneo hilo lina vyumba viwili vya kidijitali na kumbukumbu, vyumba viwili vya kusikilizia sauti na eneo la kumbukizi.

Wadau wa Taasisi za Kitaifa na washirika katika Mradi huo ni Shirika la Utangazaji Tanzania, Makumbusho ya Taifa ya Tanzania, Kumbukumbu za Taifa za Tanzania na Mfuko wa Mwalimu Nyerere kwa kushirikiana na Programu ya Urithi wa Afrika ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Maelezo:

UNESCO Dar Office, Tanzania | Nancy Kaizilege | +255 789 288 730| nk.kaizilege@unesco.org